

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI  
SHULE YA SEKONDARI KILABELA  
S. L. P 316, BARIADI – SIMIYU  
(Barua pepe: kilabelasecondaryschool2933@gmail.com)**

**SIMU NO. 0782636822**

---

**KUMB. Na. KSS/S2933/JI/2021/.....**

**MZAZI/MLEZI WA.....**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE  
YA SEKONDARI KILABELA 2021**

Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika **Shule ya Sekondari Kilabela mwaka 2021.**

Shule ya sekondari kilabela inapatikana katika **Halmashauri ya wilaya ya bariadi vijijini, Tarafa ya Nkololo, Kata ya Banemhi, kijiji cha Kilabela.** Karibu kabisa na shule ya msingi **Kilabela B.**

Shule ni ya kutwa na mchanganyiko (wavulana na wasichana). Pia shule ina mazingira mazuri ya kujifunzia.

Shule ya sekondari Kilabela inamichepuo ya **Sanaa na Sayansi.** Awapo shuleni atajifunza masomo tisa (9) ambayo ni: **CIVICS, HISTORY, GEOGRAPHY, ENGLISH, KISWAHILI, BASIC – MATHEMATICS, CHEMISTRY, BIOLOGY na PHYSICS**

Shule inatarajiwa kufunguliwa tarehe: **11/01/2021.** Hivyo anatakiwa kufika shuleni tarehe: **04/01/2021** kwa ajili ya usajiri akiwa na **mahitaji yote muhimu.**

**MAHITAJI MUHIMU**

**WASICHANA**

- 1) Shati mbili za rangi nyeupe zenye mikono mifupi.
- 2) Sketi mbili za rangi ya Bluu bahari (Light blue) zenye **rinda boksi.** Ndefu hadi kwenye **kifundo** cha mguu **“Ankle”.**
- 3) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi (Jozi mbili).
- 4) Soksi nyeupe (Jozi mbili).
- 5) Jezi ya rangi ya Bluu bahari kwa ajili ya michezo.
- 6) Sweta moja la rangi ya Bluu bahari (Light blue).

**WAVULANA**

- 1) Shati mbili za rangi nyeupe zenye mikono mifupi.

- 2) Suluali mbili za rangi ya Bluu bahari zenye mifuko mitatu; miwili mbele na mmoja nyuma. Vile vile iwe na marinda manne mbele; mawili kulia na mawili kushoto. Pia iwe na “Turn up” chini na upana wakutosha (isiwe model).
- 3) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi (Jozi mbili).
- 4) Soksi nyeusi (Jozi mbili).
- 5) Jezi ya rangi ya Bluu bahari kwa ajili ya michezo.
- 6) Sweta moja la rangi ya Bluu bahari.

#### **MAHITAJI KWA WAVULANA NA WASICHANA**

- 1) Dafutari kubwa 10 (Counter Books; **2 Quire**)
- 2) English Dictionary na Kamusi kwa somo la Kiswahili.
- 3) Mathematical set moja.
- 4) Picha ndogo (passport size) mbili.
- 5) Faili moja kwa ajili ya kuhifadha taarifa zake mbalimbali.
- 6) Mche mmoja wa mti wa matunda wa kudumu. *Mfano: muembe, mchungwa, mfenesi, nk.*

**NB:** Maelekezo haya yameambatana na;

1. ***Sheria na Kanuni za shule.*** Zisome kwa umakini, uzielewe na kuzifuata.
2. ***Medical Examination Form.*** Ijazwe na Mganga Mkuu wa Wilaya na kurejeshwa shuleni wakati wa usajiri.

Karibu sana!

.....  
**CHECHE, B.P**  
**MKUU WA SHULE**

#### **NAKALA KWA:**

1. MKAGUZI MKUU WA SHULE,  
KANDA YA MAGHARIBI,  
S. L. P 1025,  
**TABORA.**
2. AFISA ELIMU (M),  
S. L. P 4,  
**BARIADI-SIMIYU.**
3. MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
S. L. P 109,  
**BARIADI-SIMIYU.**
4. AFISA ELIMU SEKONDARI,  
S. L. P 109,  
**BARIADI-SIMIYU.**